**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**021** **KISWAHILI**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3:00** **Jumatatu, 02 Novemba 2015 asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.

2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni lazima.

3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 10)**
**UFAHAMU**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Ustaarabu ni jambo jema ambalo hupendwa na kila jamii yenye **utashi** hapa duniani. Kila jamii yenye ustaarabu mambo yake huendeshwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu zinazoeleweka. Maamuzi na mafanikio mbalimbali miongoni mwa wanajamii hutolewa bila **hamaki** wala kukurupuka. Kanuni na taratibu hizo huiongoza jamii kufikia upeo wake kimaendeleo kuanzia ngazi za chini kabisa ambayo ni familia mpaka ngazi ya juu kabisa ambayo ni taifa. Taratibu na kanuni hizo huwekwa katika chombo kimoja maalumu kinachoitwa katiba.

Katiba ni jumla ya sheria, kanuni na taratibu fulani zilizokubaliwa kuwekwa na jamii au taifa fulani kama dira ya maisha ya kila siku ya jamii au taifa hilo. Taifa bila katiba ni sawa na behewa la garimoshi bila injini. Hivyo katiba ina umuhimu wa kipekee katika taifa lolote lile.

Katika nchi zenye utamaduni wa kidemokrasia, katiba huundwa kutokana na maoni ya wananchi wake kwa utaratibu maalumu uliowekwa na serikali. Aghalbu, maoni na mawazo yaliyotolewa na wananchi huwa ni chimbuko la katiba hiyo. Wananchi hujiona ni sehemu ya utawala. Kwa upande wa pili wa sarafu, nchi zenye utaratibu wa **kiimla**, katiba hutayarishwa na watawala kwa maslahi yao binafsi. Katiba hutumiwa kama sera kwa maslahi ya watawala. Maoni na mawazo ya wananchi hayazingatiwi katika kuunda katiba.

Umuhimu wa katiba huonekana na kujidhihirisha waziwazi katika maisha ya kila siku ya nchi yoyote ile. Kwanza, katiba huelekeza wajibu wa ila mwanajamii kwa taifa lake na wajibu wa viongozi walio madarakani kwa wananchi au raia. Pili, katiba huonesha na kuainisha haki ambazo kila raia anastahili kupata na pia taratibu za kufuata katia kudai au dupewa haki hizo. Mbali na hayo, katiba hutoa utaratibu wa jinsi ya kuwapata viongozi wetu katika ngazi mabalimbali za kisiasa na kijamii. Pia uhuru wa mtu binafsi hulindwa na katiba. Hivyo, katika nchi ambayo ina katiba inayokidhi matarajio ya wananchi wote mambo huwa mazuri na kamwe chombo hakiwezi kwenda **mrama**.

Aidha, wananchi hawana budi kuelewa maana ya katiba ili waweze kutoa maoni na mapendekezo ya kuunda katiba mpya au kuimarisha iliyopo. Ni muhali kwa mtu asiyejua maana ya katiba kutoa maoni kuhusu katiba. Wananchi hupaswa kuelimishwa kupita semina, warsha na makongamano mbalimbali ili kujua katiba zao na kutoa maoni kuhusu uundaji wa katibu mpya.

Hata hivyo, wananchi wengi hasa vijana hawajitumi katika kuzijua katiba za nchi zao au kutoa maoni ya uundaji wa katiba mpya. Athari zake ni kutojua haki zao za msingi na kuburutwa kama mkokoteni na watawala katika mambo mbalimbali. Vilevile hulalamikia mambo ambayo hawakuchangia mawazo.

Hivyo basi, ni vizuri kwa wananchi kutambua, kuthamini na kuheshimu uwepo wa katiba kama kiongozi kizuri katika kuonesha njia muafaka ya kujiletea maendeleo kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kwa nchi husika.


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

**Maswali**

(a) Toa maana ya maneno yote yaliyokolezwa wino kama yalivyotumika katika habari uliyosoma.

(b) Kwa mujibu wa habari uliyosoma, taja mambo mazuri mawili yatokanayo na uwepo wa katiba katika nchi.

(c) Kwanini mwandishi anasema katiba hutumiwa kama sera kwa maslahi ya watawala?

(d) Je, ni hofu gani aliyonayo mwandishi dhidi ya vijana kuhusu katiba?

(e) Andika kichwa cha habari uliyosoma kisichozidi maneno matano (5).

2. Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua mia moja (100).

## SEHEMU B (Alama 25)
## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Watumiaji wa lugha ya Kiswahili hufanya makosa mengi bila ya kudhamiria. Taja aina mbili za makosa hayo kwa kutoa mfano wa sentensi mbili kwa kila kosa.

4. (a) Eleza maana ya rejesta.

   (b) Kwa kutoa mifano, taja mambo muhimu matatu yanayomwongoza mtumiaji wa lugha katika uteuzi wa rejesta.

5. Katika kila sentensi andika neno moja lenye maana sawa na maelezo ya sentensi husika.
   (a) Mtu anayechunguza uhalifu.
   (b) Ng'ombe dume aliyehasiwa.
   (c) Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma.
   (d) Mti unaozaa matunda yanayotengenezwa kinywaji cha kahawa.
   (e) Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzungukwa na bahari katika sehemu zake tatu.

6. Eleza dhima za mofimu "li" kama ilivyotumika katika sentensi zifuatazo:
   (a) Shamba letu li kubwa sana.
   (b) Wlishelewa kurudi.
   (c) Tunalifuatilia.
   (d) Limeharibika.
   (e) Shikilia.

7. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi:
   (a) Ameshiba sana.
   (b) Watoto wengi wanaogelea.
   (c) Mvua ilinyesha kwa wingi sana.
   (d) Kijana anakula chakula kingi.
   (e) Mimi nasoma polepole.


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (Alama 10)**
**UANDISHI**
Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Jifanye wewe ni Gudhah Mukish anayeishi mtaa wa Tandamti - Gerezani Kariakoo na unataka kuuza gari yako aina ya TOTYOTA CARINA. Andika tangazo kwenye gazeti la Mwananchi.

9. Andaa kadi ya mwaliko kwa rafiki zako ili washiriki katika mahafali ya kumaliza Kidato cha Nne yatakayofanyika shuleni kwako siku ya Jumamosi tarehe 21/11/2015, kisha kufuatiwa na tafrija fupi itakayoandaliwa na wazazi wako katika ukumbi wa Kijiji mnamo saa 10.00 jioni. Jina lako liwe Sili Silali wa SHule ya Sekondari Kiriche.

**SEHEMU D (Alama 10)**
**MAENDELEO YA KISWAHILI**
Jibu swali la **kumi (10)**

10. Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA) ni miongoni mwa taasisi zilizojitahidi katika kukuza na kueneza Kiswahili Barani Afrika. Eleza majukumu matano ya chama hiki katika kufanikisha azma hiyo.

**SEHEMU E (Alama 45)**
**FASIHI KWA UJUMLA**
Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

**ORODHA YA VITABU**

| | | |
|---|---|---|
| **Ushairi** | | |
| **Wasakatonge** | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| **Malenga Wapya** | - | TAKILUKI (DUP) |
| **Mashairi ya Chekacheka** | - | T.A. Mvungi (EP & D.LTD) |
| **Riwaya** | | |
| **Takadini** | - | Ben J. Hanson (MBS) |
| **Watoto wa Maman'tilie** | - | E. Mbogo (H.P) |
| **Joka la Mdimu** | - | A.J. Safari (H.P.) |
| **Tamthiliya** | | |
| **Orodha** | - | Steve Reynolds (MA) |
| **Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe** | - | E. Semzaba (ESC) |
| **Kilio Chetu** | - | Medical Aid Founda |

11. Kwa kutumia mifano, fafanua kanuni muhimu nne za utunzi wa mashairi ya kimapokeo.

12. "Kazi za fasihi hufichua mivutano iliyopo katika jamii." Kwa kutumia hoja tatu kwa kila diwani fafanua mivutano hiyo kutoka katika diwani mbili ulizosoma.


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

13. "Mandhari iketeuliwa vizuri humsaidia mwandishi katika kufikisha yale aliyokusudia kwa jamii yake" Thibitisha hoja hiyo kwa kutoa mifano mitatu toka katika kila kitabu kati ya riwaya mbili zilizoorodheshwa.

14. Kwa kutumia tamthiliya mbili miongoni mwa zilizoorodheshwa eleza jinsi waandishi walivyoonesha athari za utamaduni wa kigeni katika maadili ya jamii ya kiafrika.

15. (a) Vigano ni nini?

    (b) Tunga vigano kwa kutumia methali isemayo "Umdhaniaye siye kumbe ndiye!"


Mtihani huu na mitihani mingine inapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org